# PACENY COMPANY LIMITED

**Tel/Mob:** 0748 059 687 P.O.BOX 46306, **DAR ES SALAAM**

**TAR:** 31/05/2021

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Uvinza,
S.L.P 12, Uvinza,
**Kigoma.**

**Yah: Maombi ya Shamba la Ekari 375 kwa Ajili ya Uzalishaji wa Mafuta ya Chikichi.**

Tafadhali husika na kichwa cha barua hapo juu. Kampuni ya Paceny Company Limited yenye namba ya usajili 152056133 iliosajiliwa kwa sharia ya makampuni (2002) tarehe 26/05/2021 ni kampuni inayojihusisha na shughuli za kilimo, uzalishaji na usindikaji wa bidhaa zinazotokana zao la chikichi.

Paceny Company Limited imeshafanya mazungumzo na kituo cha uwekezaji nchini, Tanzania Investment Centre (TIC). TIC iliishauri Paceny Company Limited kutafuta uhakika wa kupewa shamba ili baaada ya hapo taratibu husika za kuwekeza ziendelee.

Kwa niaba ya kampuni ya Paceny Company Limited ninapenda kuwasilisha maombi ya kupewa shamba kwa ajili ya kilimo cha chikichi lenye ukubwa wa ekari 375 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya chikichi kibiashara na kuongeza tija kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na mamlaka husika za Tanzania.

Kampuni ya Paceny Company Limited inatarajia kuanza shughuli, kutekeleza taratibu na mpango wake wa kilimo biashara mara baada ya kuthibitishiwa uwezekano wa kupewa shamba.

Wako katika ujenzi wa taifa,

PACENY COMPANY LIMITED
P.O.BOX 46305
DAR ES SALAAM

..............................
Pascal Nyabenda
Mkurugenzi, Paceny Company Limited

Scanned by CamScanner

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZAMITAA
MKOA WA KIGOMA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA**

UVINZA DISTRICT COUNCIL

## FOMU YA MAOMBI YA SHAMBA LA MICHIKICHI

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA
S.L.P 12
**UVINZA-KIGOMA**

## 1.0 TAARIFA BINAFSI ZA MWOMBAJI

Jina: Paceny Company Ltd Anwani: BOX 46306, DAR ES SALAAM

Simu: 0748059687 Mahali anapoishi: DAR ES SALAAM

Kata: Ilala/Boma Wilaya: Ilala Mkoa: DAR ES SALAAM

Saini ya Mwombaji: [signature]

Naomba kununua shamba la ukubwa wa ekari 375 kwa ajili ya kilimo cha zao la Michikichi katika eneo lililotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma..

## 2.0 MASHARTI KWA MUOMBAJI:

i) Kwamba muombaji anatakiwa kulipia fomu ya maombi kwa gharama ya shilingi 20,000/= na malipo haya hayatarejeshwa (non refundable) kwa mwombaji.



Scanned by CamScanner

ii) Kwamba, Shamba utakalopewa ni kwa ajili ya kilimo cha zao la michikichi tu na itakuwa kwa maelekezo maalum kutoka kwa maafisa ugani kuchanganya mazao mengine ikihitajika katika shamba hilo.

iii) Fedha za maombi zilipwe banki ya **NMB** kupitia **Control number kwa Akaunti number 51610003362** jina la akaunti **UVINZA DC COLLECTION A/C**, number za watoa huduma za **control namba 0689881314 / 0753987045, 0764242079 / 0783904008**

iv) Kwamba, Mwombaji ambaye maombi yake yatakubaliwa atatatikiwa kulipia gharama za shamba litakalopimwa, kusafishwa, kupandwa miche ya michikichi na lenye hati ndani ya muda wa miezi 2 tu kuanzia tarehe ya kukubalika kwa maombi yake.

v) Kwamba, waombaji watume maombi kwa kuzingatia jedwali la vitalu vya mashamba hapa chini.

| S/N | Ukubwa wa Mashamba (Ekari) | Gharama kwa kila Shamba (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | 5 | 3,831,342 |
| 2 | 10 | 7,592,590 |
| 3 | 20 | 15,115,090 |

vi) Kwamba, mwombaji ambaye atashindwa kulipia gharama **ZOTE** zilizopangwa kulingana na ukubwa wa shamba aliloomba hadi mwisho wa muda uliotolewa atanyang'anywa na kupewa mtu mwingine na hatarudishiwa fedha atakazokuwa amelipia.

vii) Kwamba, mwombaji atakayekuwa amekamilisha malipo ya shamba aliyoomba atakabidhiwa shamba likiwa limepandwa michikichi ya kisasa aina ya TANERA na kukabidhiwa **HATI MILIKI** ya shamba hilo.

viii) Kwamba, mwombaji baada ya kukabidhiwa shamba lake atalazimika kuendelea kuhudimia kwa kuzingatia ushauri wa maafisa ugani.

ix) Kwamba, malipo tajwa hapo juu yanajumuisha gharama za umilikishaji wa eneo.



Scanned by CamScanner

x) Fomu iliyokamilika na nakala ya stakabadhi ya malipo irudishwe ofisi ya Manunuzi ya Halmashauri ya Wilaya Uvinza au kwa kutumia **emails:** ded@uvinzadc.go.tz masolwasalum@gmail.com, na mariagwiboha@gmail.com

xi) Mchanganuo wa gharama za mashamba (Block) ambazo mkulima/muwekezaji atatakiwa kulipia kabla ya kukabidhiwa shamba lake.

| Ukubwa wa Block (Ekari) | Gharama za kusafisha shamba na kupanda michikichi (Tshs.) | Gharama za Umilikishaji (Tshs) | Gharama za Upimaji | Gharama za kununua shamba (Tshs.) | Jumla ya Bei kwa Shamba (Block) (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | 2,545,000 | 126,342 | 160,000 | 1,000,000 | 3,831,342 |
| 10 | 5,090,000 | 182,590 | 320,000 | 2,000,000 | 7,592,590 |
| 20 | 10,180,000 | 295,090 | 640,000 | 4,000,000 | 15,115,090 |

xii. Kwa mawasiliano zaidi usisite kuwasiliana na;

1. Mkurugenzi Mtendaji
   Halmashauri ya Wilaya Uvinza
   **Email:** ded@uvinzadc.go.tz
   **Simu: 0767355345**

2. Afisa kilimo
   Halmashauri ya Wilaya Uvinza:
   **Email:** masolwasalum@gmail.com
   **Simu: 0783782222**



Scanned by CamScanner

# MASHARTI YA KILIMO CHA MICHIKICHI

Waombaji wote watakuwa na wajibu wa kuzingatia masharti ya kilimo cha michikichi kama yalivyo ainisishwa hapa chini:

i) Kwamba, Shamba utakalopewa ni kwa ajili ya kilimo cha zao la michikichi tu na itakuwa kwa maelekezo maalum kutoka kwa maafisa ugani kuchanganya mazao mengine kama ikihitajika katika shamba hilo.

ii) Kwamba mkulima atahakikisha anafuata maelekezo ya Wataalamu wa kilimo kwa kila hatua kwa mfano kufyeka, kupulizia dawa, kuweka mbolea, kupalilia kwa wakati n.k

iii) Kwamba, mwombaji atakayepata shamba katika eneo lililotengwa na Halmashauri atalazimika kuwa mwanachama chama cha msingi (AMCOS) kitakachoanzishwa katika eneo hilo la mashamba.

iv) Kwamba, mwombaji ambaye atashindwa kulipia gharama **ZOTE** zilizopangwa kulingana na ukubwa wa shamba aliloomba hadi mwisho wa muda uliotolewa atanyang'anywa na kupewa mtu mwingine na hatarudishiwa fedha yoyote atakayokuwa amelipia.

v) Kwamba, mkulima anaahidi kufuata masharti yote ya kilimo cha michikichi na endapo atashindwa kutekeleza Halmashuri itakuwa na haki ya kulitwaa shamba na kumpatia mtu mwingine.

vi) Kwamba, usafishaji wa mashamba, upimaji na uandaaji wa hati, pamoja na upandaji wa miche ya michikichi utafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza tu.

vii) Kwamba Mkulima hatoruhusiwa kupanda mashamba kwa kutumia miche ya ya michikichi ya kienyeji katika mashamba yaliyotengwa.

Mimi Paschal Nyabenda nimesoma na kuelewa vizuri, bila ya kulazimishwa na mtu yeyote, nikiwa na akili timamu nimekubali kufuata masharti yote yaliyoainishwa hapo juu.

Imesainiwa mbele ya Kamishna wa viapo (WAKILI/HAKIMU)

JINA: Edna J. Mahala

SAINI: [signature]

WADHIFA: Wakili wa Serikali

STATE ATTORNEY
0 JUN 2021
P.O. BOX 430
KIGOMA



Scanned by CamScanner

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**

Ada ya maombi imelipwa kwa stakabadhi Na. [ ] Tarehe: [ ]

Ndugu: [ ] Amekubaliwa / Amekataliwa ombi la shamba kwa ajili ya kilimo cha zao la michikichi katika eneo lililotengwa na Halmashauri ya Wilaya Uvinza.

**Maoni/Maelezo**...........................................................................................
..................................................................................................................
..................................................................................................................
..................................................................................................................

Kamishina wa Ardhi/ Afisa Mteule [ ]

Saini: [ ] Tarehe: [ ]



Scanned by CamScanner

Ardhi copy.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA**

**16 JUNI 2021**

Unapojibu tafadhali taja:
**Kumb. Na. UDC/L10/10/IV/82**
MKURUGENZI,
PACENY COMPANY LIMITED
S.L.P 46306,
**DAR ES SALAAM**

**YAH: MAOMBI YA SHAMBA LA EKARI 375 KWA AJILI YA UZALISHAJI WA MAFUTA YA CHIKICHI.**

Barua yako isiyokuwa na Kumb. Na. ya tarehe 31/05/2021 juu ya mada tajwa hapo juu yahusika,

2. Kwa barua hii ninakutaarifu kuwa maombi yako ya kuomba shamba la ekari 375 kwa ajili ya kilimo cha Chikichi yamekubali. Shamba hili litakuwa ndani ya eneo la mashamba Vitalu ya Kilimo cha Chikichi yaliyobuniwa na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ili kuongeza uzalishaji wa zao la chikichi.
3. Kama ulivyowahi kugusia katika mawasiliano kwa nyakati tofauti baina yako na Afisa Kilimo wa Wilaya Ndg. Salum Masolwa (Mhandisi.) kuwa kampuni yako ina hadhi ya kampuni ya Kigeni kwa sababu ya wanahisa wake wengi kutokuwa raia wa Tanzania, ninakuomba sasa kuwasilisha nyaraka zifuatazo ili Ofisi yangu ijiridhishe na kuanza hatua stahiki za kutimiza azima yako.
    - MEMART ya Kampuni
    - Cheti cha usajili wa kampuni
    - Annual return/Detailed information toka BRELA
    - Uthibitisho uraia wa wana hisa wa Kampuni
    - Uthibitisho wa uraia wa wakurugenzi wa Kampuni

Nakutakia utekelezaji mwema.

Ach.Weja L.Ng'olo
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
**UVINZA**

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA

Jengo la Utawala: Mtaa wa Lugufu, S.L.P 12, Uvinza/Kigoma. Simu No; +255 028 280, Nukushi; No; 028 280.
Baruapepe: [illegible] Tovuti; http://www.uvinzadc.go.tz

Scanned with CamScanner